**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

# SERA YA MSAADA WA KISHERIA

**2017**

**KWA MASHIRIKIANO:**

EUROPEAN COMMISSION

UNDP

## YALIYOMO

TAMKO LA WAZIRI ........ 1
DIBAJI ........ 2
**SURA YA KWANZA** ........ 3
1.0 UTANGULIZI ........ **3**
1.1 HISTORIA ........ 3
1.2 MAANA YA JUMLA YA MSAADA WA KISHERIA . ........ 4
**SURA YA PILI** ........ **5**
HALI HALISI YA MSAADA WA KISHERIA ZANZIBAR ........ 5
2.0 UTANGULIZI ........ 5
2.1 MFUMO WA KITAASISI WA MSAADA WA KISHERIA. ........ 5
2.2 MFUMO WA KISHERIA. ........ 6
2.3 UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA ........ 8
2.4 VIGEZO VYA WANAOSTAHIKI KUPATA MSAADA WA VISHERIA NA VIWANGO VYA WATOAJI WA MSAADA WA KISHERIA ........ 9
2.5 UWELEWA WA MSAADA WA KISHERIA ........ 10
**SURA YA TATU** ........ **11**
3.0 SABABU, DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA ........ 11
3.1 SABABU ........ 11
3.2 DIRA ........ 11
3.3 DHAMIRA ........ 11
3.4 LENGO KUU ........ 11
3.5 MALENGO MAHSUSI ........ 12
**SURA YA NNE** ........ **12**
4.0 MAENEO, HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA ........ 12
4.1 4.1 MAENEO YA SERA ........ 12
4.2 HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA ........ 12
**SURA YA TANO** ........ **16**
5.0 KAZI NA MAJUKUMU YA WAHUSIKA WA SERA. ........ 16
5.1 SERIKALI KUU ........ 16
5.2 BARAZA LA WAWAKILISHI ........ 16
5.3 OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA ........ 16
5.4 IDARA YENYE DHAMANA YA MSAADA WA KISHERIA ........ 16
5.5 POLISI, WAENDESHA MASHTAKA NA MAJAJI ........ 17
5.6 WIZARA INAYOHUSIKA NA FEDHA NA MIPANGO ........ 17
5.7 SEKTA BINAFSI, JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI, JUMUIYA ZA KIRAIA, JUMUIYA ZA KIDINI, ........ 17
5.8 TAASISI ZA ELIMU ........ 17
5.9 WATAALAMU WA SHERIA ........ 17
5.10 WASHIRIKA WA MAENDELEO ........ 18
5.11 WANANCHI KWA JUMLA ........ 18
5.12 WASAIDIZI WA SHERIA ........ 18
**SURA YA SITA** ........ **18**
6.0 UTEKELEZAJI WA SERA, UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 18
6.1 6.1 UTEKELEZAJI WA SERA. ........ 18
6.2 UFUATILIAJI NA TATHMINI. ........ 18
6.3 MAPITIO YA SERA. ........ 18

## TAMKO LA WAZIRI

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejikubalisha kuhakikisha wananchi wote wananufaika kupata haki sawa kwa kuweka misingi ya msaada wa kisheria ndani ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 ambayo inatoa haki ya kuwakilishwa katika mambo ya kisheria. Kwa sasa, Zanzibar haina Sera sahihi na inayoeleweka yenye kuongoza na kusimamia huduma za msaada wa kisheria. Kutokuwepo na Sera ya Msaada wa Kisheria kumepelekea kushindwa kuwezesha fursa hizi za haki ya kikatiba hasa kwa watu masikini na wenye mahitaji maalum Zanzibar.

Ukosefu wa Sera ya msaada wa kisheria umekuwa na athari kubwa ikiwemo kuzuia uwezo wa watu wasio na uwezo kifedha na wenye mahitaji maalum haki ya kudai na kufaidi haki zao. Katika jitihada zake za kuhakikisha kuwa msaada ya kisheria unapatikana kwa wananchi wake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua uamuzi wa dhati kuhakikisha kuwa huduma za msaada wa kisheria zinapatikana kwa wananchi. MKUZA II kwenye klasta ya tatu ya 'Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa' unatambua haja ya upatikanaji haki kama nguzo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kupunguza umasikini.

Hivyo basi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeandaa Sera ya Msaada wa Kisheria kwa madhumuni ya kuimarisha upatikanaji wa haki na hususan huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye mahitaji maalum katika jamii. Sera hiyo, miongoni mwa mambo mengine, itaweka miongozo ya kisheria na njia katika kuhakikisha uongozi, uratibu na usimamizi mzuri wa huduma za msaada wa kisheria Zanzibar.

Ni matumaini yangu kwamba Sera hii itaeleweka na itakubalika kama ni matokeo ya muda mrefu ya mijadala baina ya wahusika kutoka sekta na makundi mbali mbali. Tunawashukuru wawakilishi kutoka serikalini, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya na makundi ya kiraia kwa msaada wao wa kifedha na kiufundi wakati wa mchakato. Tuna hakika kwamba wahusika wote wataizingatia Sera hii kama ni nyenzo muhimu katika kukuza upatikanaji haki Zanzibar na kwa kufanya hivyo wataendelea kutoa rasilimali kwa utekelezaji na ufatiliaji na tathmini, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na sera.

**Haroun A. Suleiman – Waziri wa Nchi**

(Ofisi ya Rais ) katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**DIBAJI**

Katiba ya Zanzibar inatambua na inahakikisha haki katika kesi ambayo inajumuisha suala la msaada wa kisheria kama msingi wa haki za binadamu kwa watu wote. Kutambuliwa kwa haki hizi katika Katiba pamoja na kuingizwa katika Dira 2020, MKUZA II na Mpango Mkakati wa Wizara, ni uthibitisho wa dhati wa Serikali ya Mapinduzi na watu wa Zanzibar katika kuhakikisha inafuata misingi na viwango vya kimataifa vya haki za binadaamu. Zanzibar imepiga hatua nzuri katika mageuzi ya sheria zake na mifumo ili kuwezesha fursa ya ulinzi wa kisheria na upatikanaji haki. Hata hivyo, licha ya maendeleo haya yaliyofikiwa, jitihada zaidi zinahitajika kuhakikisha kwamba haki tayari inapatikana kwa watu maskini, wenye mazingira magumu na jamii kwa ujumla.

Sera ya Msaada wa Kisheria imeandaliwa na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na wahusika mbalimbali katika kutimiza jukumu lake la kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa watu wote. Sera hii inakusudia kuongeza kiwango cha upatikanaji wa haki kwa watu wote wa Zanzibar hasa kwa kuongeza ubora na kueneza suala la huduma za msaada wa kisheria, kuondosha vikwazo vinavyozuwia upatikanaji wa haki na kukuza uwepo na matumizi ya mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa kupitia usimamizi bora, uratibu na kupitia mtazamo wa wahusika wengi katika kufuatilia na kutathmini masuala ya huduma.

Sera ya Msaada wa Kisheria inatoa maelezo ya kina juu ya msaada wa kisheria Zanzibar; mfumo wa kisheria kwa ajili ya msaada wa kisheria; masuala kuhusu kuweza kupata na kuweza kukubaliwa huduma ya msaada wa kisheria; kazi na majukumu ya wahusika wote, na; mfumo wa kufuatilia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.

Tunaamini kwamba sera hii itaweza kutekelezwa katika mazingira ya ushiriki mkubwa na mashirikiano baina ya wahusika mbalimbali. Kwa hivyo, tunatoa wito kwa washirika wetu wote kuungana na Serikali ili kufanikisha utekelezaji wa Sera hii. Tuna hakika kwamba utekelezaji kamili wa Sera hii utachangia kuimarisha utawala wa sheria, kulinda na kuendeleza haki za binadamu na kuongeza upatikanaji wa haki kwa watu wote wa Zanzibar.

**Yakout H. Yakout – Katibu Mkuu.**

(Ofisi ya Rais ) katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 HISTORIA

Msingi wa kisheria kuhusu msaada wa kisheria Zanzibar umeelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Katiba inatambua kwa uwazi msaada wa kisheria ni haki ya msingi iliyoainishwa chini ya kifungu cha 12. Msaada wa kisheria ni haki isiyopingika inayotolewa chini ya Sheria ya Kimataifa ambayo inapaswa watu wote ulimwenguni wafaidike nayo. Msingi wa Utawala wa Sheria unataka kuwepo kwa usawa mbele ya Sheria. Hata hivyo, usawa mbele ya Sheria hautakuwa na maana bila ya kupatikana na kuwepo kwa mfumo wa utoaji haki, ufahamu wa haki na wajibu wa kisheria, uwezo wa kudai haki hizo na mfumo unaojitosheleza mtu kuwakilishwa katika dai lake. Kukosekana kwa mfumo madhubuti wa msaada wa kisheria kunawaondolea watu wasio na uwezo kifedha na wenye mahitaji maalum uwezo wa kudai haki zao. Katika juhudi zake za kuhakikisha msaada wa kisheria unapatikana kwa wananchi wake, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeonesha nia ya dhati katika utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi.

Mkakati wa kukuza Uchumi na kupunguza Umasikini Zanzibar MKUZA II unatambua haja ya upatikanaji wa haki kama ni nguzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kupunguza umasikini. Sera hii ya Kitaifa imependekeza kwamba upatikanaji wa haki lazima uwe rafiki, nafuu na wenye kupatikana kwa wakati kwa lengo la kukuza maendeleo endelevu ya kiuchumi na zaidi inasisitiza kwamba huduma za kisheria zitolewe kwa masikini na watu wenye mahitaji maalum Zanzibar.

Mbali na juhudi zilizochukuliwa na Serikali, suala la huduma za msaada wa kisheria Zanzibar limeungwa mkono na kutolewa kwenye ngazi tofauti na Asasi mbalimbali za Kisheria na Jumuiya zisizo za Kiserikali. Hata hivyo, huduma za msaada wa kisheria Zanzibar zinakabiliwa na changamoto kubwa ikiwemo usimamizi na uratibu usio mzuri ambao unazuia uwezo wa watu kudai na kupata haki na huduma za kisheria. Kizuizi hiki kinachangiwa na kutokuwepo kwa mfumo wa Sheria au Sera ya msaada wa kisheria

inayotoa muongozo kuhusu suala la huduma za msaada wa kisheria Zanzibar. Huduma za msaada wa Kisheria zimekuwa zikitolewa na Asasi za Kiraia kama vile Jumuiya zisizo za Kiserikali na Wasaidizi wa Sheria ambao wanafanyakazi bila ya kuwa na mashirikiano ya pamoja. Katika mwaka 2006 Chama cha wanasheria Zanzibar kilijaribu kurasimisha huduma za msaada wa Kisheria kwa kutayarisha rasimu ya Sheria ya utoaji wa Msaada wa Kisheria lakini Rasimu hii haikuweza kuwa Sheria na kufanya kazi.

Kwa ajili hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejizatiti kuandaa na kutekeleza Sera ya Msaada wa Kisheria ambayo inakusudia kuongeza upatikanaji wa haki na hususan huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye mahitaji maalum na kuimarisha ufanisi na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wakati. Sera itaweka miongozo na kupendekeza njia zitakazohakikisha usimamizi mzuri, uratibu wa huduma za msaada wa kisheria na zaidi kuhakikisha usimamizi na ulinzi wa haki za msingi za binaadam. Vile vile Sera itaweka njia ili kulinda haki za makundi yenye mahitaji maalum katika jamii na kuhakikisha watu wote katika jamii wanapata haki zao za msingi za kibinaadamu.

## 1.2 MAANA YA JUMLA YA MSAADA WA KISHERIA.

Msaada wa kisheria ni haki ya binaadamu na ni kipengele muhimu cha haki katika kesi. Kwa ujumla inafahamika kwamba msaada wa kisheria ni huduma inayotolewa bure au kwa gharama nafuu kwa mtu au watu, hasa masikini na wenye mahitaji maalum, hutolewa kama ni njia ya kuimarisha upatikanaji wa haki zao, kwa mfano; Taarifa za kisheria na elimu, ushauri na usaidizi wa kisheria, njia mbadala za usuluhishi wa migogoro (ADR) na/au uwakilishi wa kisheria.

Msaada wa kisheria unafafanuliwa na tamko la Lilongwe kuwa unajumuisha ushauri wa kisheria, usaidizi, uwakilishi, elimu na mifumo mbadala ya usuluhishi wa migogoro; na kwamba unajumuisha washirika tofauti, na kama vile Jumuiya zisizo za kiserikali, vyombo vya kitaaluma na Taasisi za Elimu. Tafsiri hii inatumika kwa mnasaba wa Zanzibar ambapo watu masikini, ambao hawawezi kulipia huduma za wakili, wanasaidiwa na vituo vya msaada wa kisheria vinavyoendeshwa na Jumuiya za Asasi za za kiraia na vyuo vikuu maalum.

# SURA YA PILI

## HALI HALISI YA MSAADA WA KISHERIA ZANZIBAR

### 2.0 Utangulizi

Huduma za Msaada wa Kisheria zinatatua malalamiko ya watu maskini na wenye mahitaji maalum kwa kuzingatia changamoto zinazotokana na kutomudu gharama za kisheria, ukosefu wa uwakilishi wa kisheria, mfumo wa kisheria kutokuwa rafiki na kutofahamu haki za kisheria. Hali halisi hii inaangalia mfumo wa msaada kisheria kitaasisi na kisheria, mfuko wa msaada wa kisheria, upatikanaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria, vigezo vya wanaostahiki na viwango vya wanaotoa msaada wa kisheria pamoja na uwelewa wa msaada wa kisheria.

### 2.1 Muundo wa Kitaasisi wa msaada wa kisheria.

Huduma za Msaada wa Kisheria Zanzibar zimekuwa zikitolewa zaidi na taasisi zisizo za kiserikali bila ya kuwepo na mfumo wa Sera au Sheria kutoka Serikalini. Taasisi hizi zinafanyakazi bila ya kuwa na mashirikiano ya pamoja katika utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria.

Kwa mujibu wa taarifa za Mtandao wa Watoaji wa Huduma wa Msaada wa Kisheria *(TANLAP)* za mwaka 2012 zipo NGOs (Jumuiya) mbili katika ngazi ya kitaifa zinazotoa huduma za msaada wa kisheria Zanzibar, Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar *(ZLSC)* na Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar *(ZAFELA).* ZLSC ina ofisi Unguja na Pemba, wakati ZAFELA ina ofisi Unguja tu. ZLSC inaoneka kuwa ni NGO inayoongoza katika utoaji wa msaada wa kisheria Zanzibar. Kituo hiki kinafanyakazi kwa msaada wa mashirika ya kigeni ambayo yanawapatia fedha. Huduma za taasisi hii zimeenea kwenye majimbo yote ya shamba na maeneo ya Mjini kwa Unguja na Pemba. ZLSC ilizindua programu ya Wasaidizi wa Sheria ili kusaidia kutoa msaada wa kisheria.

Zipo aina tofauti za msaada wa kisheria zinazotolewa na ZLSC. Huduma hizo zinajumuisha kuwashauri wananchi kuhusu haki zao na njia za kupita, inasaidia katika upatanishi na uandaaji wa nyaraka za kisheria, uwakilishi mahkamani katika kesi maalum, usuluhishi wa masuala ya familia na kusaidia washtakiwa.

Jumla ya wananchi 113, walihudumiwa katika mwaka 2015, kati yao 446 walikuwa wanaume na 440 walikuwa wanawake na 33 walikuwa watoto kwa unguja. Kwa upande wa Pemba, jumla ya wananchi 194 walihudumiwa kati ya hao,100 walikuwa wanaume na 94 walikua wanawake kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Haki za Binaadamu Zanzibar ya mwaka 2015,

Jeshi la Polisi Zanzibar vilevile hutoa msaada wa kisheria kupitia Mtandao wa Polisi Wanawake (TPF Net)Tanzania ulioanzishwa mwaka 2007 wenye dhamira ya kuimarisha mashirikiano miongoni mwa polisi wanawake, ndani ya jeshi la polisi na baina ya polisi na wananchi na hatimae kukuza ubora wa huduma ya msaada wa kisheria. TPF imeanzisha dawati la jinsia katika vituo vyote vya polisi Tanzania Bara na Zanzibar. Wafanyakazi wote walioteuliwa kufanyakazi katika madawati ya kijinsia kwaTanzania Bara na Zanzibar wamepatiwa mafunzo. Mwanzoni wanawake wengi ndio walioteuliwa, lakini kwa sasa maafisa polisi wote wanaume na wanawake wanatoa huduma za msaada wa kisheria katika madawati ya kijinsia.

Kwa sasa, Zanzibar, hakuna mfumo rasmi wa kitaasisi unaosimamia huduma za msaada wa kisheria. Kutokuwepo kwa mfumo rasmi wa kitaasisi kunaweza kupelekea mtafaruku katika utoaji wa huduma za msaada wa kisheria, ukosefu wa uratibu wa taasisi mbalimbali na kuhatarisha utoaji wa huduma bora. Zaidi ya hapo kutokuwepo kwa taasisi maalum inayosimamia huduma za msaada wa kisheria kunaweza kupelekea usimamizi mbovu, na inakuwa vigumu kufuatilia maendeleo na programu za msaada wa kisheria zilioanzishwa na wahusika mbalimbali.

## 2.2 Mfumo wa kisheria.

Utoaji wa msaada wa kisheria ni jukumu lililowekwa na Sheria ya Kimataifa kwa Nchi, kuhakikisha kwamba kunakuwepo mfumo mzuri wa msaada wa kisheria na kwamba uwe huru, unaopatikana, endelevu na wenye kuaminika. Ili Sheria ya Kimataifa iweze kutekelezwa katika nchi husika, nchi inabidi iwe ni sehemu ya makubaliano hayo. Zanzibar haijajitenga lakini ni sehemu muhimu ya Jumuiya ya Kimataifa na ni sehemu ya Makubaliano mengi ya kimataifa.

Mikataba ya Kimataifa inayopaswa kuzingatiwa inajumuisha; Tamko la Dunia juu ya Haki za Binaadam la 1948 (UDHR), Mkataba wa Kimataifa juu ya Haki za Kijamii na Kisiasa wa 1966 (ICCPR) na Mkataba juu ya Haki za Mtoto (CRC). Mbali na Mikataba ya Kimataifa ipo Mikataba ya kikanda ya Afrika ambayo inazitaka nchi wanachama, ikiwemo Zanzibar, kutoa usaidizi wa kisheria kwa wananchi wake. Mikataba hii ni Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binaadamu na Watu (*Banjul Charter*), Mkataba wa Afrika juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto na Itifaki ya Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binaadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika *(Maputo Protocol).*

Chimbuko la utoaji wa msaada wa kisheria Zanzibar ni Katiba ya Zanzibar ya 1984 ambayo inatoa haki ya kuwakilishwa katika mashauri yoyote ya kisheria chini ya kifungu cha 12. Haki hii inatambuliwa na Sheria mbili ya Jinai na Madai. Katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 2004 Mahkama Kuu katika usikilizaji wa kesi za jinai zinazojumuisha adhabu ya kifo kama vile kosa la kuua kwa makusudi, kuua bila ya kukusudia na kosa la uhaini inaweza kumpangia mshtakiwa aliekosa kuwakilishwa ambapo inaonekana kwamba mshtakiwa hana njia za kutosha za kuingiza wakili

Kwa upande wa kesi za madai, Sheria ya Madai ya 1917 (Amri 37, Kanuni ya 10) inatambua umuhimu wa uwakilishwaji na inampa mshtakiwa haki ya kuwakilishwa na wakili au mtu yoyote wakati wa usikilizwaji wa kesi yake. Zaidi ya hapo haki ya msaada wa kisheria imeoneshwa katika Sheria ya Watoto Nam. 6 ya 2011 chini ya kifungu cha 37(3) na kifungu cha 43 (1) (b) ambavyo vinaeleza kwamba kila mtoto ana haki ya kupata usaidizi wa kisheria.

Kwa sasa, Zanzibar haina Sheria maalum ambayo inasimamia na kuongoza suala la huduma za msaada wa kisheria. Kutokuwepo kwa Sheria maalum na yenye kufahamika inayoongoza huduma za msaada wa kisheria kumepelekea kushindwa kufanikisha fursa ya haki na huduma na kuingiza sharti hili la kimataifa katika sheria za ndani na kuweka viwango vinavyohusiana na huduma za utoaji wa msaada wa kisheria. Hali hii imepelekea kushindwa kuanzisha haki na wajibu kwa watoaji wa huduma za kisheria, vigezo na viwango pamoja na usimamizi mzima wa huduma za msaada wa kisheria.

## 2.3 Upatikanaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejidhatiti kuona kwamba wananchi wote wanapata haki ya msaada wa Kisheria bila ya ubaguzi kwa kuweka msingi wa kisheria katika Katiba ya Zanzibar ya 1984. Hata hivyo, upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria Zanzibar unakabiliwa na vikwazo ambavyo vinahitaji kutatuliwa kwa haraka. Kama ilivyoripotiwa awali kwa sasa kuna Jumuiya mbili tu ambazo ni *ZAFELA* na *ZLSC* zinazojihusisha na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria Zanzibar. Hata hivyo, kutegemea Jumuiya mbili tu kutoa msaada wa kisheria nchi nzima kunaleta shaka ya kuweza kuendelea. Vile vile inakuwa ni vigumu kuona jinsi gani Jumuiya (NGOs) nyengine zingeweza kujenga uwezo na uzoefu wa kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa kipindi kifupi.

Kinyume na Chama cha wanasheria wa Tanganyika, Chama cha Wanasheria Zanzibar ni Jumuiya isiyo ya Kiserikali na si taasisi iliyoanzishwa na Sheria na wala hakitoi huduma za msaada wa kisheria moja kwa moja au huduma za kisheria bila malipo. Sheria ya Mawakili Sura ya 28 Sheria za Zanzibar inawataka mawakili kutoa huduma ya msaada wa kisheria bila ya malipo, lakini hakuna kanuni maalum ya utekelezaji wa agizo hili hivyo kupelekea kutokuwepo mfumo wa bila malipo ulioandaliwa kwa mawakili. Hata hivyo Mahkama Kuu ya Zanzibar inawapangia mawakili kufanya kazi ya kuhudumia kisheria hasa katika kesi zinohusu maslahi ya umma.

Idadi ya watu wa Zanzibar inasimama kwenye milioni 1.3, na ikiwa idadi ya watu itagawanywa kwa idadi ya mawakili wote waliosajiliwa ambao ni 404, karibu ya watu 3,217 watahudumiwa na wakili mmoja kwa mujibu wa ripoti ya binaadamu Zanzibar ya 2015. Kwa sasa, kuna idadi ndogo ya mawakili ambao wanafanya kazi za uwakili Zanzibar wachache vile vile kuhudumia mfumo wa msaada wa kisheria unaokusudiwa na sera hii. Kwa mujibu wa Ripoti hii kuna idadi ya mawakili 117 na mavakili 20 waliosajiliwa na kupewa hati za akufanyakazi zao Zanzibar. Baadhi yamawakili wanatafuta hati ya kukubaliwa uwakili lakini hawana lengo la kufanya kazi ya uwakili.

Mawakili pia hawakugawika sehemu zote za Zanzibar, ambapo baadhi ya mikoa Unguja na Pemba imekosa kuwa na wakili hata mmoja. Taarifa za kitakwimu zinaonyesha kwamba mawakili wachache waliosajiliwa ndio wanaomiliki ofisi wakati walio wengi wanafanya

kazi bila ya kuwa na ofisi. Bila ya kuongezeka Idadi hii ya wanasheria haitowezekana kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa ufanisi. Inapaswa kuzingatiwa kwamba ufanisi wa mfumo wa huduma za msaada wa kisheria unahitaji mawakili wenye ujuzi na uzoefu na wanaoweza kutoa huduma bora.

Pia kuna uhaba wa Mavakili ambao wanaruhusiwa kuhudhuria katika Mahkama za Mwanzo au Mahkama za Kadhi. Vakili ni mtu ambae ameruhusiwa kufanya kazi ya uwakili katika mhakama ya mwanzo na mahkama ya kadhi ambapo mawakili hawaruhusiwi. Kwa sasa, idadi ya mavakili ambao wanaruhusiwa kufanya kazi Zanzibar ni wane wanaowakilisha asilimia 0.004 ya idadi ya watu Zanzibar na afisi zao zipo Mkoa wa Mjini na Magharibi Unguja. Watu wanaoishi Pemba na mikoa mengine ya Unguja wanalazimika kulipa gharama za ziada kwa ajili ya kupata huduma ya Vakili. Idadi ndogo ya watu wa Zanzibar ndio wanaoishi karibu na watu wenye kufahamu mambo ya kisheria ambao wanaweza kutafuta ushauri endapo atakuwa na jambo la kisheria.

Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kimezindua programu ya wasaidizi wa Sheria ili kusaidia kutoa aina mbalimbali za msaada wa kisheria. Huduma hizo zinajumuisha kutoa ushauri wa kisheria, upatanishi na uandaaji wa nyaraka za kisheria, uwakilishi mahkamani na usuluhishi wa masuala ya kifamilia na kuwasaidia washtakiwa. Kwa mujibu Uchunguzi wa Awali wa Kusimamia mradi wa wasaidizi wa sheria wa mwaka 2011, wasaidizi wa sheria wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo kutokubalika kwao katika jamii, chuki, ubaguzi, idadi kubwa ya kesi, usafiri wa kuyafikia maeneo husika, ukosefu wa Ofisi, ukubwa wa majimbo, vitendea kazi na rasilimali fedha. Changamoto nyengine ni nyenzo za mawasiliano na utunzaji siri. Zaidi ya yote Wasaidizi wa sheria hawatambuliwi rasmi na serikali.

### 2.4 Vigezo vya wanaostahiki kupata Msaada wa Kisheria na Viwango vya Watoaji wa Msaada wa Kisheria.

Wanasheria wanaweza kutoa Msaada wa Kisheria iwapo tu wataidhinishwa na chombo maalum cha kisheria. Ili waidhinishwe, ni lazima wafikie vigezo maalum vinavyohusu sifa, uwezo na uzoefu pamoja na mifumo ya utendaji. Wanatakiwa kuonesha uwezo na utaalamu kwa kutoa mifano ya kesi, sampuli za kazi zao na marejeo. Uzoefu wa nchi nyengine

unaonesha kuwa Wanasheria na Wasaidizi wa sheria kuweza kutoa msaada wa kisheria, wanahitaji kuthibitishwa na lazima wawe na mkataba wa huduma. Watoaji wote wa msaada wa kisheria lazima watekeleze mkataba na kufuata viwango vya utekelezaji kwa mujibu wa mkataba. Viwango vya utekelezaji vinaweka viwango vya chini vya utoaji huduma na maadili yanayohitajika kwa watoa huduma za msaada wa kisheria. Vilevile ni muhimu kuanzisha mfumo ambao unaweza kuwatambulisha watu wenye sifa za kupata huduma za msaada wa kisheria.

Kwa sasa, wanasheria ambao wanahitaji kufanya kazi ya uwakili Zanzibar wanapaswa kuomba kukubaliwa mbele ya Jaji Mkuu. Tofauti na mamlaka nyengine kama Tanzania Bara ambapo wanasheria wanapotaka kufanya kazi ya uwakili wanatakiwa kufanya mtihani ili waweze kukubalika kufanya kazi za uwakili, kwa Zanzibar sharti hilo halipo. Zaidi ya hilo, hakuna sharti la kisheria kwa wanasheria kuonesha uwezo na uzoefu wao wakati wanapoomba kukubaliwa kufanyakazi ya uwakili. Hakuna kinachowazuia wanasheria hawa kutoa baadhi ya huduma za msaada wa kisheria kama vile kutoa uelewa wa masuala ya kisheria kabla ya hata kukubaliwa kufanya kazi za uwakili na Jaji Mkuu. Mwanya huu wa kisheria unapelekea wanasheria kutoa huduma hizo bila kuongozwa na kusimamiwa hivyo, mamlaka zinashindwa kutambua ubora wa huduma wanazozitoa. Aidha, hakuna mfumo ulioanzishwa rasmi wa kuonesha aina ya watu wanaostahiki kupewa huduma ya msaada wa kisheria.

## 2.5 Uwelewa juu ya Msaada wa kisheria.

Uwelewa juu ya Msaada wa kisheria ni muhimu sana katika upatikanaji wa haki. Kwa mujibu wa utafiti mdogo uliofanyika Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu nyenzo za huduma za msaada wa kisheria mwezi Machi 2012, idadi kubwa ya wanajamii wa kawaida hawana uelewa juu ya kuweza kupata huduma za msaada wa kisheria. Wengi wao wenye uelewa ni wale walionufaika na msaada wa kisheria. Matokeo haya ya tafiti yanaonesha ufahamu mzuri wa wateja na watoa huduma za msaada wa kisheria. Kiwango kikubwa cha watu kutoelewa ni kuwa hawajawahi kutaka au kupata ushauri au usaidizi wa kisheria. Kwa kawaida watu hutafuta huduma hii pale wanapopata matatizo. Kukosekana kwa uelewa juu ya msaada wa kisheria kunapelekea kutokupatikana kwa huduma za msaada wa kisheria zinazotolewa na taasisi mbalimbali.

# SURA YA TATU

## 3.0 SABABU, DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA

### 3.1 Sababu

Msingi wa Utawala wa Sheria unahitaji kuwepo na usawa mbele ya Sheria kwa namna ambayo kila raia anapata haki bila ya ubaguzi. Kwa hivyo, upatikanaji wa haki ni jambo muhimu katika kuhakikisha misingi ya Utawala wa Sheria na upatikanaji wa haki nyengine zikiwemo haki ya kuweza kujitetea vile vile ni muhimu katika kulinda misingi ya usawa na kujenga imani kwa jamii katika utaratibu wa kimahakama.

Ili kuufikia msingi wa utawala wa sheria kuna umuhimu kutoa elimu juu ya haki na wajibu wa kisheria na kwa namna gani ya kudai haki hizi nakuweza mtu kuwakilisha madai yake kwa ufanisi kuhusu stahiki. Ni ukweli kwamba, kukosekana kwa mfumo madhubuti wa msaada wa kisheria kunawakosesha watu wasio na uwezo kifedha na wenye mahitaji maalum uwezo wa kudai haki zao.

Uanzishwaji wa mfumo wa msaada wa kisheria unakubaliwa kama ni njia ya utekelezaji wa kufikia matokeo yaliyopangwa katika MKUZA II. Kwa mtazamo huo, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imetayarisha Sera ya Msaada wa Kisheria ili kuweka mfumo wa utoaji na usimamizi wa huduma za msaada wa kisheria Zanzibar ili kwenda sambamba na matakwa ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

### 3.2 Dira

Watu wote waliopo Zanzibar wanapaswa kupata haki kwa sababu ni haki yao ya kikatiba.

### 3.3 Dhamira

Kutoa msaada wa kisheria kwa utaalamu, ufanisi na wakati kwa watu wasio na uwezo na wenye mahitaji maalum Zanzibar.

### 3.4 Lengo kuu

Lengo kuu la Sera ni kuweka mfumo endelevu wa upatikanaji haki kwa watu wote ili kwenda sambamba na viwango vya haki za binaadamu vya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa.

### 3.5 Malengo mahsusi

i. Kuanzisha mfumo wa kisheria na kitaasisi wa utoaji huduma za msaada wa kisheria Zanzibar.
ii. Kuanzisha programu endelevu za msaada wa kisheria na kurahisisha upatikanaji wa haki.
iii. Kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa kiwango cha ubora, ufanisi na wakati.

# SURA YA NNE

## 4.0 MAENEO, HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA

### 4.1 MAENEO YA SERA

i. Mfumo wa kitaasisi wa msaada wa kisheria
ii. Mfumo wa kisheria
iii. Uwezo na upatikanaji wa msaada wa kisheria
iv. Vigezo maalum na viwango vya msaada wa kisheria.
v. Uwelewa juu ya msaada wa kisheria

### 4.2 HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA

**Hoja ya Sera 1: Kutojitosheleza kwa muundo wa kitaasisi wa kusimamia huduma za msaada wa kisheria.**

Huduma za msaada wa kisheria Zanzibar zimekuwa zikitolewa na watu tofauti bila ya kuwepo kwa mfumo mmoja wa uratibu na usimamizi. Mawakili, Wasaidizi wa sheria na Jumuiya chache zisizo za kiserikali zimekuwa zikitoa huduma hizo pasi na kuwa na mfumo wa pamoja wa utoaji wa huduma za sheria. Kukosekana kwa Taasisi rasmi yenye jukumu la kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za sheria imepekea ugumu wa kusimamia na kufuatilia ubora na maendeleo ya huduma za msaada wa kisheria Zanzibar.

**Tamko la Sera.**

Serikali itahakikisha kuwepo kwa mfumo wa kitaasisi utakaorahisisha utoaji, usimamizi na uendelezaji wa huduma za msaada wa kisheria.

**Mikakati.**

i. Kuanzisha idara ya uratibu wa msaada wa Kisheria itakayosimamia na kutoa miongozo ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.

ii. Kuweka afisa wa msaada wa kisheria katika mamlaka za serikali za mitaa ili kuratibu huduma za msaada wa kisheria kwa ufanisi.

iii. Kuwatambulisha wawakilishi wa msaada wa kisheria katika kila shehia kufanyakazi ya huduma za msaada wa kisheria.

iv. Kujenga mkakati wa mashirikiano na washirika mbali mbali wa huduma za msaada wa sheria.

**Hoja ya Sera 2: Kukosekana kwa Sheria maalum ya huduma za msaada wa kisheria.**

Zanzibar haina sheria maalum ambayo inaweka bayana suala la usimamizi na uendeshaji wa huduma za msaada wa kisheria. Hali hii imepelekea ugumu wa kuweka vigezo, haki na wajibu wa watoaji wa msaada wa kisheria pamoja na suala zima la uendeshaji wa wa huduma za msaada wa kisheria.

**Tamko la Sera.**

Serikali itaweka mfumo wa Kisheria utakaongoza utoaji wa huduma za msaada wa kisheria Zanzibar.

**Mikakati ya sera.**

i. Kuzipitia sheria zilizopo na kutunga sheria mpya ya msaada wa kisheria.

**ii.** Kutunga kanuni za msaada wa kisheria kwa utekelezaji mzuri wa sheria mpya ya msaada wa sheria.

**Hoja ya Sera 3: Upatikanaji mdogo wa huduma za msaada wa kisheria kwa watu maskini na wenye mahitaji maalum.**

Uwezo wa kupata msaada wa kisheria huhakikisha watu wote wananufaika na haki bila ya kubaguliwa. Hata hivyo, huduma za msaada wa kisheria Zanzibar hazipatikani vyema kwa watu masikini na wenye mahitaji maalum. Kutopatikana kwa huduma hizo kunahusishwa na sababu kadhaa zikiwemo upungufu wa mawakili, vakili na mzigo wa gharama za kuajiri huduma za mawakili.

**Tamko la sera.**

Serikali itaweka mfumo utakaohakikisha huduma za msaada wa kisheria zinatosha kuweza kupatikana kwa watu masikini na wenye mahitaji maalumu.

**Mikakati ya Sera.**

i. Kuanzisha mfumo unaowatambua wasaidizi wa sheria kuwa ni watoaji wa huduma za msaada wa kisheria;
ii. Kuweka mikakati ya kuimarisha mafunzo, utoaji wa vyeti, utambuzi na motisha kwa waasaidizi wa sheria;
iii. Kushajihisha vyuo vikuu na vituo vinavyotoa mafunzo ya sheria kuanzisha vituo vya msaada wa kisheria;
iv. Kuasisi mazingira rafiki kwa wahitaji wa msaada wa kisheria kwa kurahisisha utaratibu wa kisheria na uandishi wa hati za kisheria;
**v.** Kushajihisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro.

**Hoja ya Sera 4: Kukosekana kwa vigezo vya kutambua sifa za wanaohitaji msaada wa kisheria na viwango vya watoa huduma za msaada wa kisheria.**

Kwa sasa hakuna mfumo mzuri unaowezesha kutambua wanaostahiki kupata huduma za msaada wa sheria Zanzibar. Huduma za msaada wa sheria zimekuwa zikitolewa bila ya kuwa na utaratibu maalumu, hivyo kupelekea kutokuwa na uhakika juu ya wale wanaofaa kupata msaada wa kisheria. Pia hakuna viwango vilivyowekwa kwa watoa huduma za msaada wa kisheria na hivyo mamlaka hushindwa kujua ubora wa huduma zinazotolewa.

**Tamko la Sera.**

Serikali itahakikisha panakuwepo vigezo maalum vya wanaokubalika kupata msaada wa kisheria na viwango vya watoa huduma za msaada wa kisheria.

**Mikakati ya sera**

i. Kuweka vigezo vinavyokubalika kutambua makundi ya watu wanaostahiki kupata huduma za msaada wa kisheria;
ii. Kuweka viwango vitakavyofuatwa na watoa huduma za msaada wa kisheria;
iii. Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji ili kutathmini utekelezaji kwa watoa huduma za msaada wa Kisheria na viwango vya msaada wa kisheria;
iv. Kuanzisha programu za mafunzo ili kuwapa uwelewa watoa huduma za kisheria juu ya viwango vilivyowekwa.

**Hoja ya Sera 5: Uelewa mdogo kuhusu huduma ya msaada wa kisheria.**

Upatikanaji wa haki unategemea zaidi ufahamu wa watu juu ya umuhimu na kuweza kuwepo kwa huduma za msaada wa kisheria. Wananchi wa kawaida Zanzibar wana uelewa mdogo juu ya upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria hivyo kunazuia wao kupata usaidizi maalum wa kisheria.

**Tamko la Sera:**

Serikali itahakikisha wananchi wa Zanzibar wana uelewa juu ya upatikanaji na umuhimu wa matumizi ya huduma za msaada wa kisheria.

**Mikakati ya Sera:**

i. Kutayarisha programu za uelewa wa huduma za kisheria kwa wanachi.
ii. Kufanya kampeni za ufahamu juu ya upatikanaji na matumizi muhimu ya huduma za msaada wa kisheria.

# SURA YA TANO

## 5.0 KAZI NA MAJUKUMU YA WAHUSIKA WA SERA.

### 5.1 Serikali Kuu

Wizara, Idara na Taasisi zote za serikali zina wajibu wa kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata fursa sawa ya kupata haki. Ili kufikia lengo hili, hakuna budi kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali (MDA's) kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Sera ya Msaada wa Kisheria.

### 5.2 BARAZA LA WAWAKILISHI

a) Kutunga Sheria ya Msaada wa kisheria;
b) Kufanya marekebisho ya Sheria ili ziendane na Sheria ya msaada wa kisheria.

### 5.3 OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

a) Kutayarisha rasimu ya mswada wa sheria na kutunga kanuni;
b) Kuhakikisha kwamba Wizara, Idara na Taasisi zote za serikali zinafuata Sera ya msaada wa kisheria;
c) Kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa sera ya msaada wa kisheria;
d) Kuhakikisha upatikanaji wa watendaji wenye ujuzi wa masuala ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.

### 5.4 IDARA YENYE DHAMANA YA MSAADA WA KISHERIA

a) Kutekeleza sera ya msaada wa kisheria.
b) Kuchunguza upatikanaji na ubora wa utoaji huduma za msaada wa kisheria.
c) Kutayarisha mpango Mkakati Mkuu wa utekelezaji wa sera ya msaada wa Kisheria.
d) Kutayarisha viashiria vikuu vya utendaji ili kutathmini utekelezaji wa masuala ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.
e) Kutayarisha na kufanya programu za kujenga uelewa kwa wananchi;
f) Kuwasiliana na wahusika wakuu juu ya hatua za maendeleo ya msaada wa kisheria.

## 5.5 POLISI, WAENDESHA MASHTAKA NA MAJAJI

a) Kuhakikisha kwamba watuhumiwa na washtakiwa wanajuilishwa juu ya haki ya kupata huduma za msaada wa kisheria na kuwawezesha kuwafikia watoa huduma hizo kwa haraka.
b) Kuhakikisha kwamba watuhumiwa na washtakiwa wanaweza kufanya maamuzi kwa uelewa na kwa hiari.
c) Kufanya uchunguzi wa madai yoyote kutoka kwa mtuhumiwa au mshtakiwa au watoa huduma ya msaada wa kisheria kwamba haki haikutendeka
d) Kuchukua hatua muafaka pale ambapo haki haikutendeka au inaweza kuwa haikutendeka.

## 5.6 WIZARA INAYOHUSIKA NA FEDHA NA MIPANGO

Kutafuta na kutenga fedha za kutosha kuhakikisha utekelezaji wa haraka na wa ufanisi wa sera ya msaada wa kisheria na mpango mkakati mkuu wa Sera hii.

## 5.7 SEKTA BINAFSI, JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI, JUMUIYA ZA KIRAIA, *JUMUIYA ZA KIDINI, nk.*

a) Kuchangia na kutoa msaada katika bajeti ya msaada wa kisheria
b) Kuzingatia kanuni za msaada wa kisheria na miongozo.
c) Kuzitumia ipasavyo huduma za msaada wa kisheria.

## 5.8 TAASISI ZA ELIMU

a) Kuendeleza mbele masuala ya msaada wa kisheria katika elimu na programu stadi za mafunzo.
b) Kuanzisha vituo vya msaada wa kisheria.

## 5.9 WATAALAMU WA SHERIA

a) Kutambua wajibu wa kimaadili wa kutoa huduma za msaada wa kisheria na kazi bila malipo na hivyo kukuza na kuimarisha mfumo kwa nia ya kuufanya uwe wa lazima kwa mawakili wote;
b) Kuheshimu Kanuni na viwango vya msaada wa kisheria.

### 5.10 WASHIRIKA WA MAENDELEO

Kuisaidia serikali kifedha na kiufundi katika kuendeleza huduma za msaada wa kisheria.

### 5.11 WANANCHI KWA JUMLA

a) Kuzitumia huduma za msaada wa kisheria kwa njia iliyo bora na ya ufanisi.

b) Kushiriki kikamilifu katika programu za kukuza ufahamu juu ya masuala ya msaada wa kisheria.

### 5.12 WASAIDIZI WA SHERIA

a) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa watu Masikini na wenye mahitaji maalum.

b) Kushirikiana na wahusika wengine wa msaada wa kisheria.

# SURA YA SITA

## 6.0 UTEKELEZAJI WA SERA, UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 6.1 Utekelezaji wa Sera.

Wizara inayoshughulikia masuala ya sheria itasimamia utekelezaji wa Sera ya Msaada wa Kisheria. Washirika wengine watakua na jukumu na wajibu wa pamoja katika utekelezaji wa sera hii. Idara yenye dhamana ya kushughulikia Msaada wa Kisheria itakuwa na jukumu la kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sera pamoja na kuratibu utekelezaji wake.

### 6.2 Ufuatiliaji na Tathmini.

Sera ya Msaada wa Kisheria ili itekelezwe kwa ufanisi itategemea mfumo madhubuti wa ufatiliaji na tathmini. Idara inayoshughulikia Msaada wa Kisheria itakuwa na jukumu la kutayarisha mfumo wa ufatiliaji na tathmini (M&E). Ripoti ya ufatiliaji na tathmini itatolewa na kusambazwa ili kuwawezesha wahusika katika ngazi zote kutoa maoni juu ya maendeleo ya sera.

### 6.3 Mapitio ya Sera.

Mapitio ya Sera ya Msaada wa kisheria yatafanywa ili kuakisi mahitaji yaliyopo pamoja na changamoto zinazokabili utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria.